JINA ……..……..…… TAREHE ……

NAMBA YAKO ……..…….…….. SAHIHI ……...

102/2
KISWAHILI: LUGHA
(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)
KARATASI YA 2
Julai /Agosti , 2010
MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA MAKADIRIO WA WILAYA YA MBOONI MAGHARIBI

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/2
KISWAHILI: LUGHA
(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)
KARATASI
MUDA: SAA 2½

MAAGIZO KWA MTAHINIWA
Jibu maswali yote.
Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa kumi. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

© 2010, Mbooni West District Joint Evaluation Test

Fungua ukurasa

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kwa makini kisha ujibu maswali yafuatayo.

Shoka alikuwa barubaru mmoja, fahali wa mtu, kavundumka; mwili na kukacha musuli. Mwili wake haukujali sulubu au kitisho chochote. Uso wake tinginya. Macho yake ni maboni yaliyojitahidi kutoka kwenye vibofu vyake, lakini hayakufuzu. Meno ya juu yameng'oka kwa hivyo mdomo wake wa chini umechomoza mbele na ule wa juu umerudi nyuma. Pua yake ni pande la nyama lenye matundu mawili ya ndonya. Nywele zake zimejenga tuta huku na huku na katikati, mlima safi unaoteleza. Nyuzo nyingi zimetengana na macho. Juu ya urembo hapa na pale ilikuwa nyeusi na ya shaba.

Shoka alikuwa ni mwenyeji pale kilabuni pa Biti Sururu. Daima anapotoka kuchuana na magunia huko bandarini hupita kwa Bi. Mpikawali kula kapile. Tena huchungulia kwake kama Selume, mamechanje, amelimudu jiko, na baada ya kujisaidia yeye rnwenyewe na wanawe, amemwekea yeye Shoka chochote. Ndipo hapoi tena pasi na kizuizi, huelemea kwa Biti Sururu kwa kunywa na tafrija nyengine.

Selume, mkewe, amechoshwa na udhia wake. Daima alilalamika kuwa hakuwa na mwanamme. Shoka ni mzuhali kwelikweli. Na ile ambayo Selume aliidhania itakuwa ndoa imara, imekuwa shakawa ya kuchezeana. Naam, Selume amechezewa na mwanamme huyu. Ametwishwa mzigo mzito asioweza kuubeba. Si mchezo kwake kujaza chungu cha kumtosha yeye na watoto wake na huyo Shoka, ambaye haleti chochote kwake lakini hodari wa kungojea kimeshapikwa apandie. Wallahi kama si wanawe, Selume asingelishika jiko, daima lingelala paka. Katu asingalijitia buibui na kutanga na njia. Lo, kachoshwa na shimiri za baruti anazoshindiliwa moyoni mwake.

"Shoka," alilalamika Selume, "wallahi nitakata pingu za uke mimi. Nitatoka nje nitarazaki. Lo! Mke n'sojua nilacho wala nikivaacho. Siku zote Selume na buibui. Imekuwa mimi kiguu na njia, kiguu na njia, hodi, hodi, hodi... Lo, nimechuna uso, napita nikiwaparamia watu weee, hata wameshanitoa maanani. Nipite nikikopa, nipite nikinyang'anya, mwanamke miye, ndio chungu nikizumbue. A-a, hatari. Toka nikikopa mpaka sikopeshwi tena. Nikaomba kiumbe mimi, hata sipewi tena. Ama kweli aliyeachwa nyuma kaachiwa mengi. Shoka mimi ni mwanamke , Vyo, sijatolewa nyongo.

"Sasa nikupe nini," alielemea Shoka. "Wewe uko ndani, mambo ya nje utayajuaje? Nikupe, nikupe, nikupe nini? Unasema maneno tu; maana yake mimi siumwi kukuona wewe mke wangu na watoto wangu mnateseka. Unayeumwa ni wewe tu! Nenda mwana kwenda."

"Kukosa huko kwa kila siku?" Selume alijitetea. "A-a, si kama pesa hupati Shoka, lakini ulevi na ... eee, pana watoto, Mume wangu, ukiingia chicha, ukitoka chicha. Na hadithi zako nazisikia nje. Dunia duara haina siri, ni uwanda wa jangwa huu, ulifanyalo liko nje".

"Sasa tunatukanana? "Shoka alifinya uso.

"A-a, tanaambizana kweli. Na kweli toka hapo chungu. Mimi ndiye niionaye adabu ya kiburi bwana."

"Utaiona, "bado, maana hujafa. Siku nitakayokutia maganjani, nitakubinginya, ndiyo siku utakayojua adabu ya kiburi."

"Lo, yasini. Sitowahi! Kwema lakini!"

"Babuwe we, dunia wasaa, utaniacha."

"Nani?"

"Wewe.""

"Mimi sikwachi taiaka, n'takwacha utimbwc na ulimwengu wako/'

"Wewe umeshakutimba na mori. "Tazama ulivyo; huna turuhani, haya zimekutoka. Hakuna zaibaki za uso. Nyooo! Hujui unachokila, hujui ulalapo wala uamkapo, wewe mbioni, ti, ti, ti, ti, ... Mwisho, mwisho mwisho wa habari, wewe mtu una nyumba na watoto, unakwenda kula mkahawani. Unaupiga wali wakoo uzuri, ukija hapa unajitia njaa ya Majuju wa Majuju. Ee, basi, inajuzu hivyo? Hakuna hata imani. Nyooo, mjalaana wewe kwa hakika, vitendo vyako! Nenda huko vilabuni, nami niache na ulimwengu wangu. Na kama wewe mwanamme kweli, taka usirudi tena kuja kula alichokichuma mkeo. Lo, huna haya wewe, ungalikuwa unazo, usingalikula chakula usichokijua kinakotoka. Lo, yasini!" Selume alikuwa akitetemeka kwa hamaki, ari na majuto. Ghadhabu ndizo zilizompa aseme maneno hayo; na utumwa, unyonge, na manyanyaso ya mwanamme. Mwisho wa maneno yake daima ulikuwa, "tumo taabani wanawake. Huu utumwa kamili. "Lakini hakujua namna gani alikuwa mtumwa. Alijiona anafuata kawaida na kanuni iliyotoka mbali ambayo imekuwa ngumu kugeuka. Haijulikani kama mila, au jambo gani.

Na mwanamke huyu alimpenda mumewe kwa udhati wa moyo wake, na shoka mwenyewe alijua haya. Labda kwa sababu hiyo ndipo -alipozidi inda na inadi. Alipoambiwa hivyo, ndipo alipotafuta pahala akajizika asipite kwake kwa muda wa wiki nzima, mpaka Selume akamtafuta, ampembejee, ndiyo arudi. Na Selume roho yake mtama; mbio atapita akimsaka, na anapomwona humshika miguu arudi nyumbani.

Maswali:

(a) Shoka alifanya kazi ya aina gani? (Alama 1)

……

……

……

(b) Kila baada ya kazi, Shoka alikwenda wapi? Kwa nini? (alama 3)

……

……

……

……

(c) Selume alitwishwa mzigo gani na mumewe ambao aliuona kuwa mzito mno? (Alama 2)

……

……

……

……

(d).Mwandishi aliposema kuwa Selume amechoshwa na shimiri za baruti anazoshindiliwa moyoni mwake, ana maana ngani? (Alama 2)

……

……

……

……

(e) Kwa nini watu walikuwa wamemtoa Selume maanani? Toa mfano mmoja kudhibitisha (Alama 2)

……

……

……

……

(f). Shoka alijiteteaje Selume alipomshambulia? (Alama 3

……

……

……

……

(g) Toa mifano miwili kuonyesha kuwa Selume alimpenda mumewe kwa dhati. (Alama 2)

……

……

……

……

2. MUHTASARI

<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatiayo</u>:

Basi lilipokuwa linalegeza mwendo kwa ajili ya kukaribia kituo chake, umati wa watu uliokuwa ukisubiri kwa amani na utulivu mara ulianza kufumkana. Kila nitu alitimua mbio kutapia nafasi chache zilizokuwamo basini. Ilikuwa mume nguvuze. Heshima, mila na utu vilitoweka kama vumbi linavyopeperushwa na upepo wa tufani. Lengo lilikuwa ni kuingia basini kwa vyovyote.

Mama mmoja aliyekuwa ameeleka mtoto, alibanwa hata karibu mtoto wake kuzimia. Kelele za mama huyu hazikumshtua mtu. Nyuma yake mzee mmoja aliyejawa na mvi kichwani alitifuliwa pu! chini! kama kidaka. Badala ya kusikitikiwa watu waliangua kicheko wakamcheka kama kinyago. Mabarobaro na vijana waliowahi kupata nafasi ya kwanza ya kujipenyeza kwa kutumia mabavu waliweza kujibarizi katika viti vichache vilivyokuwa vitupu. Hawakujali akina mama waja wazito wala waliobeba watoto migongoni waliokuwa wamesimama huku wamebanwa. Na wazee waliokuwa wamesimama huku mikono yao ikitetemeka pia hawakutiwa maanani na mtu.

Kabla ya watu hawajatulizana dereva aliliondosha gari kwa nguvu na mfululizo wa mabuyu makali. Basi lilikuwa halijapata hatua, wakati kelele za abiria na wapita njia ziliposikika zikimkemea dereva, 'we! unaua dereva! simamisha gari! simamisha gari!' Ilichukua muda kidogo hata gari liliposimama. Akili yote ya dereva ilikuwa ni kulitimua basi ili aokotee abiria walio njiani na kuwashindilia garini; Shabaha kubwa ilikuwa ni pesa si huduma kwa watu.

Hatimaye basi liliposimama jamaa wawili makamu walikuwa wamekwisha hasirika. Mmoja wao alianguka na kukanyagwa na gari iliyokuwa nyuma yake. Miguu yake yote miwili ilivunjwa kenyekenye. Wa pili aliyekuwa akilewalewa alianguka pia lakini hakuumia sana. Milolongo ya magari iliyokuwa nyuma ya basi ilikwama, kungojea polisi waje wachunguze ajali iliyofanyika. Badala ya madereva wa magari yaliyokwama kusikitishwa na ajali iliyotukia, walianza kufyoa; kila mmoja alikuwa ameghadhibika kwa 'kucheleweshwa

bure'. Hakuna aliyejali kuwa yule mtu atakufa au atapona. Hakuna aliyemlaumu dereva kwa taadi zake wala mshika pesa kwa kushindilia watu basini bila kujali. Hapana shaka hapa pana hatari kubwa ya kuweka pesa na ubinafsi mbele ya ubinadamu.

(a) Fupisha aya ya pili kwa maneno 40-45 (Alama 6)
Matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

(Utiririko alama 1)

(b) Kwa maneno 55, eleza yaliyotokea basi liliposimama (Alama 7)
Matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

(Utiririko alama 1)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Akifisha sentensi ifuatayo (Alama 1)
Unyonge wa masikini uliishia papo kwa domo kaya. Ina maana gani.

……

(b) Taja konsonanti mbili ambazo hujulikana kama nusu irabu. (Alama1)

……

(c) Andika sentensi mbili ukitumia neno mwizi kama: (Alama 2)
(i) Kivumishi

……

……

(ii) Jina

……

……

(d) Tunga sentensi ya neno moja iliyo na visehemu vifuatavyo (Alama 2)
i) Nafsi

……

ii) Wakati

……

iii) Kirejeshi

……

iv) Kitendewa

……

v) Shina la kitenzi

……

vi) Kauli ya kutendea

……

vii) Kimalizio

……

(e) **Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo** (Alama 1)

Darasa lao halikuwa na milango mikubwa ya kupitia.
Anza : Milango mikubwa……..

……

(f) Kwa kutungia sentensi, tofautisha kati ya viwakilishi nafsi. (Alama 2)

……

……

……

……

(g) Tungia sentensi kiungo kifuatacho ili kudhihirisha maana ya dhana katika mabano (Alama 2)

A (Wakati usiodhihirika)

……

……

(h) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale (Alama 3)

Wetu mmoja mfupi aliyekuwa mgonjwa anaimba vizuri.

……

……

……

……

……

……

(i) Kanusha sentensi hizi: (Alama 2)

i) Wangefika nyumbani mapema wangempata mama yao angali hai.

……

ii) Yeye akiachwa pekee ataivuruga kazi.

……

(j) Piga mstari virai katika sentensi zifuatazo na utaje aina zake. (Alama 2)

i) Mboga zilipandwa kando ya mto.

……

ii) Wanafunzi wote wazembe wataadhibiwa.

……

(k) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia kinyume: (Alama 2)

Mzee yule mfupi ni muungwana na alianika nguo za mamaye asubuhi

……

(l) Andika kwa umoja

i. Nyavu za akina mama hazishiki nguva (Alama 1)

……

ii. Andika kwa udogo

Nyoka huyu mrefu mnene ni hatari naye akikuuma utaweza kuaga dunia kwa haraka sana. (Alama 1)

……

(m) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika msemo wa taarifa

i. “Mwaka ujao nitawatembelea kwenu.” Kevin alituahidi. (Alama 1)

……

ii. “Nimepita kwake nyumbani lakini sikumwona ingawa ameniahidi kwamba hataondoka.” Ali alituarifu. (Alama 2)

……

(n) Tunga sentensi mbili ukitumia vitenzi vifutavyo katika kauli ya kutendwa (Alama2)

i. pwa

……

ii. chwa

……

(o) Andika sentensi mbili kudhihirisha tofauti ya maneno yafuatayo (Alama 2)

i. Paa / Baa

……

……

ii. Vunja / vuja

……

……

(p) Yaweke majina yafuatayo kwa ngeli zake (Alama 2)

i. Pua

……

ii. Nyangumi

……

(q) Tofautisha sentensi hizi kimaana: (Alama 2)

i. Ningekuwa na uwezo ningesafiri kwenda ng'ambo

ii. Ningalikuwa na uwezo ningalisafiri kwenda ng'ambo

……

……

……

……

(r) Tunga sentensi yenye yambwa tendwa na yambwa tenda (Alama 2)

……

……

……

……

(s) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya `KI` (Alama 2)

……

……

……

……

(t) Tunga sentensi mbili zenye vikundi tenzi hivi (Alama 2)

i. Kitenzi, nomino na kitenzi

ii. Kitenzi na kitenzi

……

……

……

……

(u) Tofautisha kati ya kiimbo na shadda (Alama 1)

……

……

……

……

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a. Lahaja ni nini? (Alama 2)

……

……

……

……

b. Eleza kuhusu chanzo cha lahaja (Alama 4)

……

……

……

……

……

……

……

……

c. Fafanua mambo manne yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili barani Afrika Mashariki katika karne 18 na 19. (Alama 4)

……

……

……

……

……